

ASb
approved

Nyumba Ya Kobe

Brigid Simiyu
Katrien Coetzer



Kiswahili



Siku moja, Kobe alikuwa
akitembea nyanini.
Alichunguza mbele na
kukodolea nyasi macho
akamwona Konokono.

"Unatafuta nini?" Konokono alimuuliza. "Ninatafuta nyumba yangu. Umeiona?"



Alijibu, "La, sijaiona, lakini nitakusaidia kuitafuta!" Konokono alipanda juu ya gamba la Kobe. Kobe alimbeba Konokono mgongoni mwake. Walitafuta, lakini hawakuiona.



Baada ya muda mfupi,
walimwona Chiriku.
"Mnatafuta nini?" Chiriku
aliwauliza. "Ninatafuta
nyumba yangu.
Umeiona?" Kobe alisema.
"La, sijaiona, lakini
nitakusaidia
kuitafuta!" Chiriku akajibu.



Chiriku aliyapapatua
mabawa yake na kupaa.
"Unakwenda kwa kasi
sana." Kobe alilalamika.
Chiriku akamwambia,
"Samahani, wacha nami
pia niruke juu ya gamba
lako."



Kobe aliwabeba Konokono
na Chiriku juu ya gamba
lake. Walitafuta bila kuona
ishara ya nyumba ya
Kobe.



Walipoendelea,
walimwona Bunzi.
"Mnatafuta nini?" Bunzi
aliwauliza. "Ninatafuta
nyumba yangu.
Umeiona?" Kobe alijibu.



Bunzi alisema, "La, sijaiona, lakini nitakusaidia kuitafuta!" Aliruka mgongoni mwa Kobe. Kobe aliwabeba Konokono, Chiriku na Bunzi. Walitafuta, lakini hawakuona nyumba yoyote.



Hatua chache, walikutana na Panya. Alikuwa akitengeneza shada zuri la maua. "Unatafuta nini?" Panya aliuliza. "Natafuta nyumba yangu. Umeiona?" Kobe alisema.



Panya alijibu, "La, sijaiona, lakini nitakusaidia kuitafuta!" Aliruka mgongoni mwa Kobe. "Subiri, siwezi kuacha maua yangu." Panya alijinyoosha, akayakusanya maua yake huku Kobe akimsubiri.



Kobe aliendelea kutembea
akiwabeba Konokono,
Chiriku, Bunzi na Panya
mgongoni mwake.
Walitafuta, lakini
hawakuipata nyumba ya
Kobe. Upepo
uliyapeperusha maua ya
Panya. Kobe alikuwa
amechoka sana. Akasema,
"Ninyi ni wazito."



Upepo uliongezeka. Anga likabadilika likawa jeusi. "Ah, iwapi nyumba yangu?" Kobe aliuliza. Punde, radi ilinguruma milimani na umeme ukaangaza. Mara mvua ikaanza kunyesha. "Ah, iwapi nyumba ya Kobe?" Konokono, Chiriku, Bunzi na Panya waliuliza.



Upepo ulizidi kuvuma na kuvuruga. Ghafla, upepo uliwapeperusha wote kutoka mgongoni mwa Kobe.



Mvua ya mawe ikaanza kunyesha. Kwa uoga, Kobe alijikunja na kuingia ndani ya gamba lake. Mle ndani mlikuwa joto. "Kumbe, hii ndiyo nyumba yangu!" Kobe aliwaza.



Konokono, Chiriku, Bunzi
na Panya walijikusanya
chini ya gamba la Kobe
wakatambua, "Ah, hii
ndiyo nyumba ya Kobe!"

Nyumba Ya Kobe

Author - Maya Fowler

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Katrien Coetzer

Language - Kiswahili

Level - First paragraphs

© Katrien Coetzer, Maya Fowler, Damian Gibbs, Bookdash.org and African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.bookdash.org